

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**FOMU YA MKATABA WA UJENZI KWA FUNDI**

**A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA**

1	MWAJIRI	Mkuu wa Chuo  Chuo cha ualimu wa Ufundi stadi Morogoro  S. L. P. 671 Morogoro  Kny: <i>VOCATIONAL TEACHERS TRAINING COLLEGE</i> Katibu Mkuu <i>P. O. BOX 671 MOROGORO</i> Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia
2	JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa)	Jina: ..... <i>ELIANA... NHAMBI</i>  Anwani: .....  Simu: ..... <i>0766 - 955525</i>
3	ENEO LA UJENZI	MVTTC - MOROGORO
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	KAZI YA UMEME WA JENGO LA BWENI LA WASICHANA (TYPE ONE)
5	GHARAMA YA UFUNDI (+ Skills Development Levy):	Tshs. MILIONI MBILI NA LAKI TANO (2,500,000)
6	MUDA WA MKATABA  (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Tarehe ya Kusaini .. <i>25/11/2021</i>  Muda: <i>81k/Do</i> (Taja idadi siku)  Tarehe ya Kuanza Kazi .. <i>15/12/2021</i>  Tarehe ya Kumaliza Kazi .. <i>25/04/2022</i>
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Hakuna Malipo ya Awali</li> <li>• Fundi atalipwa kwa awamu <i>5</i> baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa</li> </ul>

### B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi (*kama inavyooneshwa katika kijeduari hapa chini*) na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

#### 3.1 Jeduari la mchanganuo wa kazi Umeme.

MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI YA UFUNDI UMEME JENGO LA BWENI  
LA WASICHANA  
JINA LA FUNDI ..... *F. KANYA MLAMBI*

MCHANGANUO GHARAMA WA KAZI ZA UMEME KATIKA JENGO LA BWENI LA WASICHANA		
NA	KAZI	GHARAMA
1. Kufanya wiring na accessories zake kwenye jengo la Bweni La Wasichana (kuweka mfumo mpya wa umeme kama mchoro unavyoonyesha na maelekezo utakayopewa na msimamizi wa kazi)		
a. kuchimbia mabonba na kuweka box za swichi	750,000	
b. kufanya wiring jengo zima	1,000,000	
c. kusunga taa, ac, feni, swich n.k kama ilivyo kwenye mchoro	750,000	
JUMLA YA GHARAMA ZA UFUNDI		<b>2,500,000</b>
JUMLA KUU (GHARAMA ZA KAZI + KODI)		<b>2,500,000</b>

4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsinamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kuijenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

7. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu ye yote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Ucheleweshaji wa Kazi:
  - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.
11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:
  - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (*kutokana na fedha au vifaa*), Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.
12. Uvunjwaji wa Mkataba:
  - Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vyta ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
  - Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

13. Maelekezo ya kazi yatatolewa na msimamizi mkuu wa kazi (Clerk of works) na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia msimamizi wa kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyoifanya itakaguliwa na kufika angalau 30%.

MWAJIRI:

Saini: ..... Ephrem

Jina: Ephrem Matambi

Cheo: Kaimu M/Chuo

Tarehe: 25/11/2021  
PRINCIPAL  
VOCATIONAL TRAINING COLLEGE  
P.O. Box 877  
MOROGORO

FUNDI:

Saini: ..... FUNDI

Jina: FUNDI

Cheo: EIKANX MLAMBI

Tarehe: 25/11/2021

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: And

Jina: ANDREW D. RD

Cheo: ICIMWI MIWU WA  
MFUNZO

Tarehe: 30/11/2021

SHAHIDI WA FUNDI

Saini: Afumany Mnandi

Jina: Afumany

Cheo: FUNDI

Tarehe: 25/11/2021